

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA KILIMO**  
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**

Kumb. Na. AC.118/319/01

05 Julai, 2023



**TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA YA MUDA YA UDEREVA NA AFISA  
MILIKI MALI II**

Bodi ya Korosho Tanzania imepata kibali cha kuajiri kwa muda nafasi Sita (6) za Udereva na Moja (1) ya Afisa Miliki Mali II kupitia barua ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yenye Kumb. FA.10/01'F'/134 ya tarehe **09 Mei, 2023**

**1. AFISA MILIKI MALI II (1)**

**A. SIFA ZA WAOMBAJI**

- (a) Awe Mtanzania mwenye umri kati ya Miaka 18 hadi 40;
- (b) Awe amehitimu kidato cha VI ; na
- (c) Awe na Shahada ya Uhandisi wa Majengo, Ukadiriaji Majengo au Mchumi wa Majengo.

**B. MAJUKUMU YA KAZI YA AFISA MILIKI MALI II**

- i. Kuhakikisha nyumba zote na majengo ya Bodi ya Korosho yanatunzwa na kuwa kwénye hali Nzuri;
- ii. Kupanga na kutoa ushauri wa namna nzuri ya kufanya maboresho nyumba na majengo yote ya Bodi;
- iii. Kufuatilia ukarabati ya miundombinu yote ya majengo ya Bodi ya Korosho Tanzania;
- iv. Kuhakikisha usalama wa majengo ya Bodi ya Korosho baada ya kufanya matengenezo makubwa au kazi za ukarabati;
- v. Kuhakikisha kazi za ukarabati na ujenzi zinafanyika kwa ufanisi, gharama nafuu na kukakamilika kwa wakati;
- vi. Kufuatilia na kuhakikisha kwamba Viwanja vyote vilivyojengwa au ambavyo viko wazi vinasimamiwa ipasavyo dhidi ya uvamizi;
- vii. Kutoa ushauri juu ya namna bora ya matumizi na uendelezaji wa rasilimali zilizopo katika kuongeza kipato cha taasisi;
- viii. Kufanya kazi zingine zote atakazopangiwa na Mkuu wa Idara yake.

**Mshahara**

Mshahara wa Afisa Miliki Mali II kwa mwezi ni Tsh 650,000/=

## **2. MADEREVA SITA (6)**

### **SIFA ZA MUOMBAJI**

- (a) Awe Mtanzania mwenye umri kati ya Miaka 18 hadi 40;
- (b) Awe amehitimu kidato cha Nne na kufaulu Kiingereza na Kiswahili;
- (c) Awe amesoma **TRADE TEST GRADE II/ DRIVER GRADE II**/ Cheti kutoka katika taasisi inayotambulika na Serikali; na
- (d) Awe na Leseni ya Udereva ilio hai **Daraja C, C1, C2, au C3** ambaye hajawahi kupata ajali katika miaka mitatu (3) iliyopita.

### **MAJUKUMU YA KAZI YA UDEREVA**

- (a) Kuendesha gari ya Bodi ya Korosho atakayopangiwa;
- (b) Kuhakikisha gari atakayopangiwa inakuwa katika hali nzuri muda wote;
- (c) Kutunza na kuweka kumbukumbu za safari pamoja na matengenezo kwenye kitabu cha kumbukumbu za gari;
- (d) Kutunza na kuhakikisha usalama wa gari muda wote na kutoa taarifa kwa haraka pale zinapoitokeza dalili za hitilafu zozote katika gari;
- (e) Kuzingatia taratibu za matengenezo ya kawaida kwa kufuata ratiba kulingana na umbali ambao gari limetembea;
- (f) Kufanya matengenezo madogo kwenye gari kwa ruhusa ya Afisa Rasilimali Watu; na
- (g) Kufanya majukumu mengine yoyote atakayopangiwa na msimamizi wake.

### **Mshahara**

Mshahara wa dereva kwa mwezi ni Tsh 450,000/=

**AJIRA HII NI YA MKATABA WA MWAKA MMOJA NA SIO YA KUDUMU.**

**Maombi yote yatumwe kwa anuani hii kabla ya tarehe 12.07.2023 saa 10:00 jioni.**

MKURUGENZI MKUU,  
BODI YA KOROSHO TANZANIA,  
S.L.P 533,  
**MTWARA**  
Barua pepe: [info@cashew.go.tz](mailto:info@cashew.go.tz)

***“Bodi ya Korosho ni Mwajiri anaezingatia Fursa sawa kwa Wote”***